



## Utangulizi

Imani ni nini? Imani inaweza kuelezewa kuwa ni kuwa na mtumaini kikamilifu bila ya mashaka (a) Mungu, kuwa ndiye anaye timiza ahadi zake zilizomo kwenye neno lake; na (b) Yesu Masihi (Kristo) kuwa ni Mwokozi na Bwana. Imani inatusaidia kuuona ukweli wa kile kisichoonekana. Ni hali endelevu kwa Mkristo wa Kweli.

Mungu amejidhihirisha kikamilifu ya kwamba yeye anaaminika. Tunamuamini Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, kwasababu aliishi maisha ya ukamilifu, akituonyesha jinsi ambavyo tunapaswa kuishi kwa utii. Yesu Kristo alilipa deni letu lililotokana na uasi wetu dhidi ya Mungu (dhambi), na alifanya hivyo kwa kuishi bila ya kutenda dhambi na kisha kufa msalabani kwaajili yetu. Tunamuamini mwana wa Mungu kwasababu alienda msalabani kwa hiari huku akijua akawa sadaka kamilifu kwa wanadamu wote, na pia sadaka kamilifu kwa kila mmoja wetu binafsi. Tuna imani kwasababu Mungu hutimiza ahadi zake. Tanaamini kwasababu Mungu amempenda kila mwanadamu licha ya kuwepo dhambi ambazo mara kwa mara huleta uharibifu. Je ametupendaje? Kwa kumtoa mwana wake Yesu Kristo kuchukua nafasi yetu. Upendo wake si kwasababu tuna uzuri wowote ama 'tunastahili' kupendwa. Kwasababu ya rehema zake ametupatia ile zawadi tusiyostahili. Nia yake ni kwamba kila mmoja wetu asiendeele kuwa mtumwa wa dhambi, ila(kupitia kwa Yesu) tuokolewe kutoka katika adhabu, nguvu na madhara ya dhambi. Waumini wa Kikristo wanatiwa moyo kupitia majibu ya sala zao na kupitia nguvu ya ucha Mungu tunazoziona tukitazama maisha wa maisha ya watu wengine wanaoweka imani yao kwa Bwana Yesu.

Hivyo basi tunasababu nzuri ya kuwa na imani. Mapenzi ya Mungu ni kwamba imani yetu iongezeke – na huu ndiyo unaonekana kwa muda mwingi kuwa ni muundo, wa wale wanaotembea karibu na Mungu na kufuata njia zake.

## Katika Agano la Kale

Wokovu kwa njia ya imani unaonekana mara kwa mara. Pia kuna imani halisi katika ahadi na makubaliano na Mungu ya mara kwa mara. (makubaliano haya huitwa 'agano'). Vifuatavyo ni baa-dhi ya vifungu vya Agano la Kale vinavyozungumzia juu ya imani na muendelezo wa maelezo yake katika Agano Jipya.

Mwanzo **6:22**; **12:1-5**; **13:14-18** rejea Waebrania **11:7-10**

Mwanzo **15:6** rejea Warumi **4:2-5**; Waebrania **11:11-12**

Mwanzo **22:1-19** rejea Waebrania **11:17-19**

Mwanzo **50: 24, 25** rejea Waebrania **11:22**

Kutoka **9:20, 21**; Kutoka **12: 21-25** rejea Waebrania **11:28**

Joshua **6:20** rejea Waebrania **11:30**

Ruthu **2:12**; Zaburi **56:3**

## Katika Agano Jipya

Yesu Kristo alidai kuwa ametimiza ahadi za Agano la Kale.

Kwaajili hiyo, tangu hapo na kuendelea hadi sasa, imani inapaswa kuelekezwa kwake.

Mathayo **16:8**; Marko **6:5-6**; **9:23**; **10:52**; Luka **7:50**; **8:50**; **17:5-6**; **22:32**

Yohana **1:12**; **3:15-16**, **36**, **6:35-36**; **7:38**; **8:24**; **11:25-26**; **12:46**

Mitume walitoka na kwenda ulimwenguni wakiwa na ujumbe mmoja: “Muamini Bwana Yesu nawe utaokolewa” (matendo **16:31**).

Matendo **3:16**; **4:12**; **8:5**, **35**; **10:43**; Warumi **3:21-22**; **5:1-2**; **10:4**, **9**; 1Wakorintho **1: 23**; **2:2**; 2 Wakorintho **4:5**

Wagalatia **2:15-16**, **20**; **3:22**; 2 Wathesalonike **1:3**; 1 Petro **1:8**, **21**; **2:7**

## Tunaokolewa kwa neema kwa njia ya imani

Lakini matunda ya imani hii yataonekana katika matendo ya maisha yetu. Imani peke yake haina thawabu – ni mikono yetu inayopokea wokovu unaotolewa na Mungu.

Warumi **4:1-5**; **10:9-10**; Yakobo **2:14**, **16**, **24**; Tito **3:4-8**; Wagalatia **2:21**; Waefeso **2:8-10**; **6:16**

1 Timotheo **6:12**; 1 Yohana **5:4**

## Ufupisho wa Biblia

Wingu la mashahidi walioishi na kufa katika imani.

Waebrania **12:1-2** (rejea sura ya 11)

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK  
www.sovereignworldtrust.org.uk

### Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - www.christian-publications-int.com  
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron- Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons  
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission  
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4